بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

23Dulqa'da 1444H

12/06/2023M

# UFAFANUZI KUHUSU MAKALA YETU

## 'CHUKUA TAHADHARI DHIDI YA NJAMA ZA RIBA'



Assalaam alaikum warahmatullah wabarakatuh. Shukran kwa mwongozo huo mzuri Sheikh. Sasa sielewi miamala halali ya biashara ni ipi hasa? Bank hizo zinafanya miamala yake kwa kukupa huduma au bidhaa na si pesa. Mfano ni kama huo uliotolewa hapo. Kama unataka kununua gari au kujenga nyumba unatakiwa kupeleka hati ya madai (invoice/profoma) na wao watalipia hiyo huduma nawe utalipa kidogo kidogo kwa ongezeko ambalo wao husema ni faida katika muamala husika. Je tutafanya biashara kwa mtaji gani usio na riba? Naomba unisaidie maana nahitaji kukopa lakini naogopa "RIBA" SHEIKH.

JAWABU

Waalaikumu ssalaamu warahmatullaah wabarakaatuh.

Hilo ni swali la ndugu yetu ambaye amesoma makala yetu tuliyoituma katika grupu letu la MARKAZ IBNU UTHAIMIN DODOMA inayozungumzia kuchukua tahadhari dhidi ya njama za riba. (Rejea makala hiyo hapo juu). Muulizaji ana maswali mawili ya msingi; Miamala halali ya biashara ni ipi hasa? Je tutafanya biashara kwa mtaji gani usio na riba?

Tutazingatia zaidi nukta ambayo ndiyo sababu ya kuulizwa maswali hayo kisha tutaashiria majibu ya maswali hayo kwa uchache pamoja na kumuomba ndugu yetu aendelee kufuatilia makala zetu za miamala ya kibiashara na kadhalika .

Nukta ya msingi ni hiyo iliyopo kwenye mfano alioutoa muulizaji kwamba : Kama unataka kununua gari au kujenga nyumba unatakiwa kupeleka hati ya madai (invoice/profoma) na wao watalipia hiyo huduma nawe utalipa kidogo kidogo kwa ongezeko ambalo wao husema ni faida katika muamala husika.



Katika muamala huu, miongoni mwa mambo ya msingi kufahamu kwa undani ni kwamba: je ni kweli Bank hizo zinafanya miamala yake kwa kukupa huduma au bidhaa na si pesa. ?

Uhalisia wa muamala huu ni mkopo wa pesa ambao benki inamkopesha mtu ambaye hana pesa ya pamoja ya kununua gari au kiwanja kisha benki hiyo badala ya kumkabidhi mkononi pesa hiyo yule muhitaji wa gari , inamkabidhi muuzaji wa gari au kiwanja moja kwa moja. Kisha mkopo huo unatakiwa ulipwe zaidi ya kiwango cha awali ambacho muhitaji wa gari amekopeshwa. Huu ndio uhalisia wa muamala huo, na wala si kama inavyoweza kufahamika kwa harakaharaka kwamba Bank hizo zinafanya miamala yake kwa kukupa huduma au bidhaa na si pesa.

Miongoni mwa hoja zinazothibitisha hilo, ni kama hizi zifuatazo:

Benki haitoi hundi ya pesa ya gari au kiwanja kabla ya kumpata muhitaji wa kiwanja au gari hilo aliyeshindwa kununua gari kwa pesa yake ya pamoja. Hii ni alama ya kwamba benki haifanyi biashara ya magari au viwanja bali inafanya muamala wa kukopesha pesa kwa wale wanaohitaji kununua magari au viwanja n.k. Tunafahamu kuwa kuna makampuni na mashirika au hata watu binafsi ambao wanafanya biashara iliyo halali ya magari na viwanja na kadhalika. Wao hufanya hivi: kabla ya kuuza gari wasiokuwa nalo huwa wananunua kwanza gari hizo kwa kuagiza kutoka nje ya nchi au sehemu yoyote

hata ndani ya nchi kisha wanauza kwa wateja wahitaji wa magari hayo , sawasawa uuzaji wao uwe wa malipo ya pamoja au kwa ulipaji wa kidogokidogo.

Mfano wa muamala huo wa benki ni kama vile watu wawili ; Juma, ambaye ni mwalimu na Hussein, ambaye ni mfanyabiashara wa madini. Juma anahitaji gari linalouzwa milioni 15 lakini hana pesa ya pamoja ya kununua gari , lakini Hussein ana uwezo mkubwa wa mali lakini hamiliki magari. Juma akaelekea kwa Hussein akamwambia 'nahitaji gari lakini sina pesa ya pamoja ya kununua gari' (hali ya kuwa Juma anajua kuwa Huseein hamiliki gari ila anazo pesa za kutosha kununua gari). Hussein akamwambia Juma kwamba 'kama unahitaji gari nenda sehemu wanapouza gari ulete karatasi rasmi inayoonyesha bei ya gari hilo (invoice/profoma) ili nikununulie gari kwa makubali–ano ya kunirejeshea milioni 15 na nusu ndani ya miaka mitatu' . Juma akakubali na akafanya kama alivyoelekezwa.

Kisha baada ya Juma kufikisha karatasi ya bei (invoice/profoma) kutoka sehemu wauzayo magari , Hussein akatoa cheki / hundi ya un–unuzi wa gari kwa shilingi milioni 15. Kisha ilipofikishwa hundi hiyo kwa muuzaji wa gari, Juma akakabidhiwa gari ya shilingi milioni 15, hali ya kuwa amebaki na deni la shilingi milini 15 na nusu benki.

Maswali ya kujiuliza kwa haraka haraka;

(1) Unadhani ni kipi kilichomsukuma Juma mpaka akaelekea kwa Hussein wakati anajua Hussein hamiliki magari?

(a) Pesa za Hussein (b) Magari ya Hussein | A



(2) Unadhani gari limenunuliwa kwa cash (malipo ya pamoja) au malipo ya kidogokidogo?

(a) Malipo ya pamoja (milioni 15) (b) kidogo kidogo (milioni 15 na nusu) | A

Sababu za majibu hayo:

(1) Tumejibu kuwa kilichomsukuma Juma mpaka akaelekea kwa Hussein wakati anajua Hussein hamiliki magari, ni pesa za Hussein kwa sababu ; Juma ni muhitaji wa gari wakati huohuo hana pesa za pamoja za kununua gari hilo; kumbe anahitaji kwanza msaada wa pesa kabla ya kuelekea kununua gari katika maeneo ambayo wanauza magari. Kaelekea kwa Hussein ili akapate msaada wa pesa ya kununua gari. Isipokuwa utaratibu wa Hussein ni kwamba hatoi pesa na kuikabidhi mkononi kwa mtu bali anahitaji aikabidhi kwa muuzaji wa huduma ambayo Juma anaihitajia (gari).

(2) Tumejibu kuwa gari limenunuliwa kwa cash (malipo ya pamoja ya shilingi milioni 15) kwa sababu pesa yote hiyo imelipwa kwa pamoja. Ama kuhusu milioni 15 na nusu iliyolipwa kidogo kidogo hili ni deni lililopo baina ya Juma na Hussein halimuhusu kabisa muuzaji wa gari, kwa sababu yeye ameshapata amana yake kamilifu kwa muda muafaka.

Swali lifuatalo linajitokeza hapa:

Ikiwa uhalisia ndivyo ulivyo, kwamba gari limenunuliwa kwa cash (malipo ya pamoja) Ni nani aliyenunua gari? Je, ni Hussein au Juma? Yaani Ni benki au ni mtu aliyekwenda kuhitaji huduma ya kununuliwa gari?

Hili ni swali la msingi sana kwani watu wengi wanadhanishwa kuwa mnunuzi hapo ni benki (Hussein) kwa sababu ndiyo iliyotoa pesa , na mtu anayehitaji huduma ya gari (Juma) hana pesa mkononi kwa hiyo ni kama vile benki (Hussein) imenunua gari kwa shilingi milioni 15 kisha ikaliuza kwa (Juma) shilingi milioni 15 na nusu. Yaani ni kama vile gari limeuzwa mara mbili kwanza limeuzwa benki kwa Tsh milioni 15 kisha benki ikaliuza gari hilo kwa Tsh milioni 15 na nusu. Dhana hii ndiyo inayoonekana katika sura ya nje bali ndio inayosambazwa na kupelekea baadhi ya watu kuamini kuwa **Bank hizo zinafanya miamala yake kwa kukupa huduma au bidhaa na si pesa.**

Kama nilivyotanguliza hapo mwanzo kusema kwamba uhalisia na uhakika wa muamala huu si biashara ya gari kati ya benki na muhitaji wa huduma ya gari bali ni mkopo wa pesa ambao benki inamkopesha mtu ambaye anahitaji huduma ya gari lakini hana pesa ya pamoja ya kununua gari. Kisha benki imekubali kumkopesha pesa kwa kuikabidhi kwa muuzaji wa gari moja kwa moja. Kwa maana hiyo huo ni mkopo ambao benki imeweka sharti la malipo ya ziada .

Tambua kuwa mkopo wowote ambao utakuwa unapelekea upatikanaji wa faida kwa mkopeshaji basi manufaa hayo ni riba, na mkopo huo ni haramu.Kama alivyosema Mtume swallallaah alaihi wasallam (( Kila mkopo unaopelekea faida (kwa mkopeshaji) ni riba)) Albayhaqiy 5/350

NB:{ Itakuja makala maalumu Inshaa Allah inayozungumzia mikopo}

Hebu tuchukulie kwamba benki ndiyo iliyonunua gari hilo kisha imeliuza kwa muhitaji wa huduma ! Ikiwa hivyo ndivyo, bado muamala huo haukusalimika, kama mwongozo wa sheria ya Uislamu ulivyo wazi ndani ya maneno ya Mtume swallallaahu alaihi wasallam yafuatayo:



(1) Alisema Hakim Ibn Hizaam Allah amridhie; ‘Ewe Mtume wa Allah amekuja mtu kwangu anataka nimuuzie kitu nisichokuwa nacho, Je nimuuzie kutoka sokoni ? Akajibu (( Usiuze usichokuwa nacho)). Abu Daud 3503.

(2) (( Yeyote atakayenunua chakula (au bidhaa yoyote) asiiuze (kwa mtu mwingine) mpaka atakapokabidhiwa )) Abu Daud 3492

Hayo ni makatazo ya kuuza bidhaa ambayo huimiliki au ipo katika umiliki wa mtu mwingine au ukawa umeinunua kwa mtu wa kwanza halafu ukaiuza kwa mtu mwingine kabla ya kukabidhiwa kutoka kwa mtu wa kwanza.

Makatazo haya japokuwa hayahusiki na riba, lakini yanahusika na uharamu na ubatili wa muamala uliofanywa katika hali kama hizo. Hivyo ikiwa muamala huu wa kibenki utasalimika na riba, hautosalimika na ubatili kwa sura hizo tulizozitaja.

Ili kusalimika na riba katika muamala huo zipo njia nyingi sana zilizo salama za kufanya kwa asiyekuwa na kipato cha kutosha kununua gari kwa malipo ya pamoja, ikiwemo njia zifuatazo;

(1) Benki inunue gari au kiwanja n.k. na ikabidhiwe kisha ndipo iuze kwa ulipaji kidogokidogo kwa wasio na cash.

(2) Anayetaka kununua gari n.k na hana pesa ya pamoja atafute wanaouza magari kwa njia ya ulipaji wa kidogokidogo kama atabahatika kuwapata.

(3) Kama hatowapata, atafute mtu wa kumkopa mkopo usiokuwa na riba (ziada).

وصلى الله على محمد وآله وصحبه وسلم

Mkusanyaji na Mkalimani: Ummati Abdallah, Abuu Muhammad